

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA ULANGA

SHULE YA SEKONDARI ULANGA.

S.L.P 31,

MAHENGE / ULANGA

.....
KWA MZAZI WA.....

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA I - 2021 KATIKA SHULE YA SEKONDARI
ULANGA.

Rejea kichwa cha habari hapo juu.

Ndugu mzazi ninapenda kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha Kwanza katika shule ya Sekondari Ulanga iliyopo Kata ya Milola kijiji cha Milola, Wilayani Ulanga. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021. Mwanao asiporipoti hadi tarehe 18/01/2021 hatua kali zitachukuliwa kwako mzazi. Mwanao afikapo shulenii anapaswa kuwa na mahitaji yafuatayo:-

A. SARE

Wasichana :

- ❖ Sketi nyeusi mtindo wa rinda box ndefu. (mbili)
- ❖ Shati jeupe mikono mifupi (mawili).
- ❖ Nusu kanzu na Hijabu nyeupe kwa Waislamu (mbili).
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba.
- ❖ Soksi nyeupe.
- ❖ Jezi ya zambarau (Mbeya city) kwa ajili ya michezo (mbili).

Wavulana:

- ❖ Suruali nyeusi yenye marinda mawili(celebrations)
- ❖ Shati jeupe mikono mifupi (miwili)
- ❖ Viatu vyeusi vya Ngozi vya Kamba.
- ❖ Soksi nyeusi.
- ❖ Mkanda wa Ngozi mweusi.
- ❖ Jezi ya zambarau (Mbeya city) kwa ajili ya michezo.

B. VIFAA VYA KUJIFUNZIA DARASANI

- ❖ Daftari 9 kubwa
- ❖ Kalamu za wino za kutosha.
- ❖ Vitabu – dictionary, vitabu vya kujifunzia kingereza (muhimu sana)

NB:Mwanao afahamu kuwa kingereza ndiyo lugha ya mawasiliano shuleni hivyo anapaswa kujifunza lugha ya kingereza na wewe mzazi unapaswa kumpa msaada wa hali na mali katika kujifunza.

C. VIFAA VYA USAFI

- ❖ Ndoo ndogo.
- ❖ Ufagio wa chelewa.

NB: Mwanao anapaswa kuwa na fagio na jembe na kwanja nyumbani. Atakuja nalo shuleni pale atakapohitajika na kurudisha nyumbani baada ya kazi ya elimu ya kujitegemea na usafi.

MUHIMU

Mwanao anapaswa kuonesha nidhamu ya hali ya juu kwa kuwaheshimu walimu, wanafunzi wenzake Pamoja na wageni na watu wote wanaofika shuleni kwani huo ndio msingi thabiti wa kujifunza na kuweza kufanikiwa.

Mwanao anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na kazi za nje ya darasa ikiwemo elimu ya kujitegemea na michezo, ili aweze kupata ujuzi mbalimbali utakao msaidia baada ya kuhitimu masomo yake hapa shuleni.

Vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu havitavumilika, hivyo wewe mzazi unapaswa kumsisitiza mwanao kufuata sheria za shule taratibu na maagizo yote ili aweze kujifunza kwa amani na utulivu.

Uongozi wa shule ya Sekondari ya Ulanga unampongeza mwanao kwa kupata nafasi hivyo tunamkaribisha mwanao shuleni Ulanga Sekondari.

"Elimu ni ukombozi, izingatie ili uiokomboe jamii yako"

Mwal. Haule V. J

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI ULANGA
S. L. P. C
MAHENGE/ULANGA